BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI, KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA UKUZAJI NA KULINDA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR NAM.11 YA MWAKA 2004 NA KUTUNGA SHERIA YA MAMLAKA YA UKUZAJI NA KULINDA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

Mheshimiwa Spika,

Naanza hotuba hii kwa kumshukuru Mola wetu Mtukufu, aliyetujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza letu Tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili hatimaye tuweze kuuchangia kwa umakini na hatimae kuupitisha mswada uliopo mbele yetu kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika,

Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa niaba ya Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo ili niwasilishe maoni ya Kamati kuhusiana na "Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 11 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo",

Mheshimiwa Spika,

Kwa namna ya pekee nachukua fursa hii adhimu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Ramadhani Hamza Chande kwa ushindi wake uliodhihirisha kwamba Jimbo la

Jang'ombe daima litaendelea kuwa jimbo la chama cha Mapinduzi na haliwezi hata kusogelewa au kuchukuliwa na Vyama vyengine vya upinzani. Kamati yetu inaungana na Waheshimiwa wajumbe wote kukukaribisha sana Baraza la Wawakilishi ili tuunganishe nguvu zetu katika kuwatumikia wananchi wetu kwa lengo ambalo Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein analieleza la kuwaletea wananchi maendeleo. Hapana shaka, Kamati yetu na Baraza kwa ujumla itakupatia ushirikiano wa hali ya juu katika utekelezaji wa majukumu yako.

Mheshimiwa Spika,

Naomba sasa nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa, Dkt. Khalid Salum Mohammed, Katibu Mkuu Ndugu Khamis Mussa Omar pamoja na timu yao ya watalaamu kwa mashirikiano yao makubwa waliyoipatia Kamati yetu katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu.

Kadhalika, napenda kuishukuru Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuanzisha utaratibu wa kutupatia dozi nzuri ya mafunzo ambayo kwa kiasi kikubwa yameweza kutupa mwangaza wa kile kilichokusudiwa kuelezwa kisheria ndani ya Mswada huu. Naomba utaratibu huo mpya uendelee kutekelezwa kwa nia ya kuongeza ufanisi wa shughuli hii muhimu ya utungaji wa sheria kupitia muhimili huu wa Baraza. Sambamba na hilo, tunawashukuru Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya Kamati.

Mheshimiwa Spika,

Nitakuwa sikuwatendea haki iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuujadili na kuuchambua mswada

ulioletwa mbele yao kwa upeo na ustadi wa hali ya juu. Naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii mmoja baada ya mwengine kama ifuatavyo:

1	Dkt. Mwinyihaji Makame	Mwenyekiti
2	Mhe. Hamida Abdalla Issa	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Masoud Abrahman Masoud	Mjumbe
4.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
5.	Mhe. Mohamed Mgaza Jecha	Mjumbe
6.	Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf	Mjumbe
7.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe

Makatib

1. Ndugu Asma Ali Kassim
2. Ndugu Said Khamis Ramadhan

Mheshimiwa Spika,

Fasili ya (6) ya kanuni ya 83 ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016 inaipa uwezo Kamati yetu kuwaalika Wadau mbali mbali kila inapotokea shughuli ya kujadili miswada ya sheria. Hivyo, Kamati iliwaalika wadau kutoka taasisi zifuatazo ili kutoa maoni yao juu ya mswada uliopo mbele yetu.

1) Jumuiya ya Asasi zisizokuwa za Kiserikali (ANGOZA);

2) Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu (Zanzibar University);
3) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Zanzibar pamoja na
4) Wadau binafsi wa masuala ya Uwekezaji Zanzibar.

Kamati inathamini michango muhimu iliyotolewa na Wadau hao na kuwashukuru kwa maoni na ushauri uliotuwezesha kuwa na uelewa mpana na ufahamu wa kina wa Mswada huu.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kuleta mswada huu katika wakati mwafaka ambapo nchi yetu imo kwenye mageuzi ya kiuchumi kutoka uchumi wa kutegemea kilimo hadi uchumi wa viwanda kupitia wawekezaji tofauti. Katika uchambuzi wa mswada ulioletwa mbele yetu, Kamati imegundua kasoro ndogo ndogo na kufanya marekebisho kwa nia ya kuuimarisha zaidi. Maeneo yaliyofanyiwa marekebisho ni haya yafuatayo:

UANZISHWAJI WA KITENGO MAALUM CHA KUTOA HUDUMA KWA WAWEKEZAJI

Mheshimiwa Spika,

wakati wa kupitia na kujadili Mswada huu, Kamati ilifarijika sana kuona kilio chake cha siku nyingi cha kuanzishwa kitengo Maalum cha kutoa huduma kwa Wawekezaji na wafanyabiashara kwa ujumla kimepatiwa ufumbuzi. Kwa kipindi kirefu Kamati yangu ilikuwa ikihimiza sana juu ya uanzishwaji wa kitengo hicho kupitia ziara zake mbali mbali ilizokuwa ikizifanya. Ni dhahiri kuwa, uanzishwaji wa Kituo hichi "One Stop Centre" utarahisisha upatikanaji wa huduma kwa Wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kuongeza ajira kwa vijana wetu kupitia sekta mbali mbali pamoja na kuinua pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na uanzishwaji wake, Kamati inazitaka Wizara na Taasisi zote zinazopaswa kuwa na Maofisa wao katika kitengo hicho, wapeleke Maofisa Waandamizi watakaokuwa na uwezo wa kutoa maamuzi kuhusu masuala yote yanayowasilishwa katika meza zao, ili waweze kutoa maamuzi yanayofaa bila kuchelewa kwa ajili ya maendeleo ya Uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 8(3) cha Mswada uliopo mbele yetu, kimeunda kitengo hicho Maalum cha kutoa huduma kwa Wawekezaji kwa kuzitaja Taasisi sita za Serikali ambazo ni: 1) Kamisheni ya Ardhi; 2) Idara ya Uhamiaji; 3) Kamisheni ya Kazi; 4) Mamlaka ya Mapato Tanzania; 5) Idara ya Udhibiti Ujenzi; na 6) Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali. Baada ya Kamati kupitia na kuchambua kwa undani kifungu hicho, iligundua kuna baadhi ya Maofisa Waandamizi ambao ni muhimu sana kuwemo hawajashirikishwa wala kuingizwa katika kitengo hicho.

Mheshimiwa Spika,

Ili chombo hicho kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ni lazima awepo Ofisa Mwandamizi kutoka Idara ya Mazingira. Afisa huyo atakua dhamana wa kufanya Tathmini ya usalama au uwezekano wa Mradi kuharibu mazingira yaani “Environmental Impact Assessment” pia kutoa ushauri wa uwezekano wa Mradi kupunguza athari hizo zisiweze kutokezea.

Mheshimiwa Spika,

Ni busara pia kitengo hicho kikamuhusisha Ofisa Mwandamizi kutoka Idara ya Majengo yaani Mtaalamu wa Majengo. Kuwepo kwa Ofisa huyo kutasaidia katika ufanyaji wa tathmini ya Miradi inayotarajiwa kuwekezwa kwa thamani halisi ya fedha na kuiepusha

Mamlaka kuingia katika migogoro mikubwa na Wawekezaji itakayoweza kuigharimu nchi yetu fedha nyingi na kuitia katika hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika,

Mbali na Maofisa hao, pia kuna haja ya kuwepo Ofisa Mwandamizi kutoka Bodi ya Mapato Zanzibar ili aweze kurahisisha kazi zote za kufanya mchanganuo wa kodi stahiki kwa wateja watakaohitaji huduma kutoka katika kitengo hicho. Kwa mantiki hiyo, Kamati yangu ina kila sababu ya kuamini kwamba watendaji hao ni muhimu sana kuingizwa katika kitengo hicho ili kurahisisha utendaji wa kitengo hicho muhimu kuwa wa umakini na wenye tija zaidi.

KUWEPO KWA KIPAUMBELE KWA BAADHI YA KAZI KUFANYWA NA WAZANZIBARI

Mheshimiwa Spika,

Kamati ilipokuwa inapitia Jadweli la Nne iligundua kuwa kuna kazi ambazo zimeorodheshwa kwa ajili ya kufanywa na Wazanzibari pekee. Hili ni suala muhimu kuwepo kwani takribani nchi zote huwa haziruhusu kazi ambazo wazawa wanaweza kuzifanya kuwapa fursa wageni kushughulika nazo. Tunaipongeza Serikali kwa kulipa uzito suala hilo na kuonesha juhudi inazochukua za kuwajali wananchi wetu na kupunguza tatizo la ajira nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika,

Licha ya dhamira nzuri ya Serikali ya kuainisha kazi hizo, Kamati yangu imeona bado kuna ulazima wa kuiongeza orodha hiyo kwa kuingiza kazi kama za nyumba ya kulala wageni; Wakala wa usafirishaji; duka la zawadi; huduma ya usafi wa nyumba au Ofisi na huduma za ulinzi wa nyumba au Ofisi zibakie zinafanywa na Wazanzibari pekee ili kero na malalamiko ya wageni kufanya kazi ambazo Wazanzibari wanazimudu yaweze kupungua kama sio kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Spika,

Suala la kipaumbele kwa baadhi ya kazi kufanywa na Wazanzibari, naomba niitake Wizara kupitia ZIPA ilisimamie na kulitekeleza kivitendo kama Mswada huu unavyoelekeza na sio kubaki na kasumba iliyoenea kwamba Wazanzibari hawawezi kufanya baadhi ya kazi. Aidha, nawaasa wananchi wetu kwamba waache desturi ya kuchagua kazi ilimradi kazi hiyo ni halali kwa mujibu wa sheria za nchi na maadili ya kizanzibari kwani waswahili wanasema "kazi ni kazi hoja mkono uwende kinywani".

KUFUTA AU KUPUNGUZA BAADHI YA VIFUNGU

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na mambo mengine, Kamati yangu iliondosha baadhi ya vifungu au maneno ambayo kwa namna moja au nyengine yameonekana yanagongana kimaana au itakuwa vigumu kuyatekeleza iwapo yataachwa na kuwemo katika Mswada huu.

Mheshimiwa Spika,

Kwa pamoja, Kamati yangu iliamua kukifuta kifungu cha 3 cha Mswada huu kinachozungumzia 'Madhumuni na Malengo ya Sheria' kwani hakioneshi ulazimu wa kubakia kwa vile maudhui yanayoelezwa katika kifungu hicho yanapatikana ndani ya kifungu cha 5 kinachozungumzia 'Madhumuni na Malengo ya Mamlaka' hususan baada ya kuingizwa marekebisho ambayo Kamati imeyapendekeza.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yetu pia imekifuta kifungu cha 34 cha Mswada huu kinachozungumzia kinga dhidi ya uchukuliwaji wa ardhi ambacho kimeonekana hakipo wazi kwa mantiki halisi ya kulinda mali za Wawekezaji wetu. Kamati imependekeza kitumike kifungu cha 22 cha

Sheria ya mwanzo ambacho kipo wazi na kinafahamika zaidi ukilinganisha na kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika,

Kamati imeliweka sawa jina la Mswada huu ili liweze kujikita na dhana nzima ambazo zinajitokeza na kuelezwa ndani yake. Kiujumla, neno 'Vitega Uchumi' ambalo ndio lililotumika katika jina letu la Mswada halija akisi picha ya Mswada wetu kwa vile halijatumika sana ndani ya Mswada huu wakati neno 'Uwekezaji' ndio neno linalofahamika na kutumika sana na kujenga taswira nzima inayokusudiwa. Mheshimiwa Spika mbali na hayo, uzoefu unaonesha kwamba Sheria nyingi ambazo Kamati imezipitia hususan za majirani zetu hapa Afrika Mashariki zinatumia neno Uwekezaji badala ya Vitega Uchumi. Kwa mantiki hayo, Kamati yangu inashawishika kulibadilisha jina la Mswada wetu ili liweze kuwa bora zaidi na kusomeka ifuatavyo: ***"Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya ukuzaji na kulinda vitega uchumi Zanzibar Nam. 11 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo."***

Mheshimiwa Spika,

Kwa upande wa Jadweli, Kamati yangu imegundua kwamba kuna baadhi ya Jadweli zinahitaji kuangaliwa upya na nyengine zifanyiwe marekebisho ya kuongeza au kupunguza masharti yaliyoelezwa ndani yake. Kwa mfano, Jadweli la Sita la Mswada huu, Kamati imependekeza kulifuta na kuandaliwa Jadweli jengine kutokana na kwamba mambo mengi yaliyomo yamejirudia au yanaonekana hayakupangwa katika mpangilio mzuri utakaoweza kusomeka na kufahamika kiurahisi zaidi. Jadweli la sita jipya linaonekana kupitia kiambatanisho ambacho Waheshimiwa mmepatiwa. Sambamba na hilo, Kamati yangu imeziunganisha na kuziongeza baadhi ya kazi ambazo zimepangwa kufanywa na Wazanzibari zikiwemo duka la vinyozi, ususi na vipodozi; duka la biashara za jumla na reja reja na uwendeshaji wa shughuli za kitalii.

UWEZO WA WAZIRI KUTUNGA KANUNI

Mheshimiwa Spika,

kifungu cha 49(2) cha Mswada huu kimeeleza uwezo wa Waziri kutunga Kanuni kuhusu utoaji wa vivutio maalum kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi yaani 'Diaspora' ambao wanataka kuwekeza Zanzibar, utaratibu wa ukataji wa rufaa na kuweka vigezo pamoja na utaratibu wa kumjuilisha au kuomba idhini ya Serikali juu ya mradi wa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika,

Tunapenda kulitanabahisha Baraza lako kwamba bila ya kuwepo Kanuni zitakazoelezea na kufafanua kwa uwazi masuala hayo, ufanisi katika uwekezaji hautopatikana. Kamati inaishauri Wizara kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba Kanuni zinaundwa mapema iwezekanavyo na kuwasilishwa katika Kamati ya Kanuni ndogo ndogo ya Baraza hili tukufu ili baadae zianze kutumika kwa maslahi ya Wawekezaji wetu.

Mheshimiwa Spika,

Kimsingi, kuwepo kwa Kanuni hizo ndio zitakazowahakikishia Wawekezaji wetu wa ndani na nje ya Zanzibar kupata haki ya kukata rufaa dhidi ya kutoridhika na maamuzi yoyote yatakayotolewa au hatua nzima za usikilizwaji na utatuzi wa migogoro pindi itapotokezea. Kamati yetu inasisitiza na kumtaka Mheshimiwa Waziri kuharakisha utungaji wa Kanuni hizo ili kuondoa wasiwasi hususan kwa Wawekezaji wa kundi la Zanzibar 'Diaspora'.

KUWAENDELEZA WANANCHI WETU KIELIMU

Mheshimiwa Spika,

Wananchi wetu wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kutokuwa na elimu ya kutosha kuweza kukidhi haja ya kutekeleza ipasavyo kazi zinazoibuliwa kutokana na Uwekezaji. SMZ kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inahitaji kuongeza juhudi za

kuhakikisha wananchi wetu hasa wanaomaliza kidato cha Nne wanatengenezewa utaratibu mzuri wa kusoma fani za kazi za vitendo (Vocational Training) au za ujasiriamali zinazoendana na rasilimali zilizotuzunguka zikiwemo uvuvi, kilimo na hata mafuta na Gesi Asilia.

Mheshimiwa Spika,

Kuna umuhimu mkubwa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, kupitia vyuo vyetu kuingiza katika mitaala yeke au kuanzisha vyuo vya mafunzo mbalimbali ambayo itawawezesha vijana wetu kumudu ushindani katika soko la ajira linalotokana na uwekezaji hususan katika masuala ya Utalii, Uvuvi na Kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yetu imebaini makosa madogo madogo na imependekeza marekebisho ya makosa ya kisarufi na kuweka uwiano baina ya mswada wa Kiingereza na wa Kiswahili yanayoonekana kwenye waraka wa mapendekezo ya marekebisho ambao Waheshimiwa Wajumbe tayari mmepatiwa.

Mheshimiwa Spika,

Mwisho naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini. Naomba Waheshimiwa Wajumbe tuuchangie, tuujadili, tutowe mapendekezo na hatimae tuupitishe mswada huu.

Mheshimiwa Spika,

Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

…….……
Dkt. Mwinyihaji Makame,
Mwenyekiti,
Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.